**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA WAZIRI MKUU – TAMISEMI**

**Namba Za Simu**
**Mkuu Wa Shule: 0629 155 082**
**0764 903 973**
**Makamu mkuu wa Shule : 0622780978**
**0767 184 204**
**Mwandamizi Taaluma: 0623 785 672**
**0758 376 248**
**Mwalimu wa Nidhamu: 0626 144 239.**
**Email : lugufuboys@gmail.com and byabushaissa@gmail.com**

**SHULE YA SEKONDARI**
**LUGUFU BOYS,**
**S.L.P 567**
**UVINZA-KIGOMA**
**Tarehe ………….**

**PICHA (PASSPORT SIZE) YA MWANAFUNZI**

**Mzazi / Mlezi wa Mwanafunzi:**

**…………………………………………………………………..**

**S. L. P ……………………….**

**YAH: MAELEZO YA KUJIUNGA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI LUGUFU BOYS HALMASHAURI YA WILAYA UVINZA MKOA WA KIGOMA KWA MWAKA WA MASOMO …………..**

1. Nafurahi kukuarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga kidato cha tano katika shule hii ya Lugufu Boys kwa mwaka wa masomo …………….. kati ya tahasusi sita tulizonazo ambazo ni PCM, PCB, HGE, HGL, HGK , HKL ni ambapo mwanao amechaguliwa Tahasusi ya___________.
   **Shule ya sekondari Lugufu Boys** ni ya Bweni ipo umbali wa kilomita 11 kusini mwa Mji wa Lugufu, ambapo ndipo makao makuu ya wilaya ya Uvinza. Pindi ufikapo Makao makuu ya Wilaya ulizia kituo cha polisi Lugufu kwa ajili ya usafiri wa kukuleta shuleni.
   Muhula wa masomo unaanza tarehe __________. Hivyo mwanao anatakiwa kuripoti tarehe -________________na mwisho wa kuripoti ni tarehe __________.
2. **Mambo muhimu ya kuzingatia**

2.1 **Sare za Shule**

(a) Sare ya Shule ni suruali nyeusi na shati nyeupe ya mikono mirefu.Mwanafunzi aje na jozi (pair) mbili au zaidi za suruali na shati.
(b) Sare za michezo ni tracksuit nyeusi zenye michirizi myeupe.
(c) Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na Kamba vyenye visigino vifupi.
(d) Mkanda wa kuvalia suruali ni mweusi usiwe na nembo au chuma kikubwa.
(e) Soksi nyeusi jozi mbili au Zaidi
(f) Sweta nyeusi .
**(g)** T.shirt (1) light bluu/bluu bahari **yenye rangi ya bendera ya taifa kwenye fito za mikono yote miwili na kwenye kola ya shingo.**
(h) Nguo za kushindia (shamba dress) T-shirt mbili za bluu zisizo na kola wala maandishi (Babalance-Grade 1 nzito) pamoja na suruali mbili za kaki.
(i) Tai nyeusi ya kitambaa cha suruali.

**NB: Mwanafunzi asije na nguo za nyumbani**

2.2 **Michango ya Shule**

2.3

(a) Michango ilipwe kwenye akaunti ya ***Shule ya sekondari Lugufu Boys , 51610003581,*** katika Benki ya ***NMB*** tawi lolote hapa Tanzania (***tafadhali andika Jina la mwanafunzi kwenye Bank Pay Slip na mwanafunzi aje nayo shuleni***).

(b) **Michango inayotakiwa kulipwa na kila mzazi kwa mwaka ni;**

| | | |
|---|---|---|
| **i.** | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | **65,000/=** |
| ii. | Tahadhari | **5,000/=** |
| iii. | Nembo | **5,000/=** |
| iv. | Kitambulisho cha Shule | **5,000/=** |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

***Jumla ya Michango 80,000/= kwa mwaka*** **(Michango Hii ilipwe kwenye akaunti ya Benki ya NMB -*Shule ya sekondari Lugufu Boys , 51610003581*) .**

**Pesa ya mkononi haitopokelewa.**

**NB: MZAZI / MLEZI ANASHAURIWA**

- **Kumkatia mwanao kadi ya Bima ya Afya ya *NHIF* ya 50,400/= na kadi hiyo aje nayo shuleni ili aweze kupata matibabu hospitali yoyote nchini.**

**MAHITAJI MUHIMU AMBAYO MWANAFUNZI WOTE WANAPASWA KULETA SHULENI NI:-**

i. Ream (3) ya karatasi kwa mwaka
ii. Vitabu vya masomo kwa tahasusi husika hasa vinavyotolewa na Taasisi ya Elimu Tanzania (TIE).Pia unaweza kuangalia baadhi ya vitabu tulivyoorodhesha kwenye kiambata cha mwisho **(Fomu namba 4 ).**
iii. **Dissecting kit na Dissecting dish** kwa wanafunzi wa Biolojia **(PCB)**
iv. Mathematical Set
v. Graph papers kwa mwanafunzi anaesoma masomo ya Science na Geography.
vi. Scientific calculator kwa wanafunzi wa masomo ya sayansi na Hisabati - fx 991
vii. Godoro lenye ukubwa wa 2½ x 6.
viii. Ndoo ndogo mbili zenye mifuniko.
ix. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe).
x. Shuka mbili rangi ya bluu,blanketi zito na chandarua chenye rangi ya bluu pembe nne .
xi. Kurunzi au Tochi.
**xii. Jezi ya michezo (Bukta na T-shirt) yenye rangi ya bluu au nyeusi na viatu vya michezo na soksi (Lazima).**

**Mahitaji ambayo kila mwanafunzi anatakiwa kuja nayo shuleni:**

- **JEMBE NA MPINI WAKE.**
- **FAGIO 2 ZA NJEE- CHELEWA.**
- **NDOO MBILI NDOGO LITA 10.**
- **MFAGIO 1 WA NDANI -SOFT BROOM .**
- **BRASHI 1 YA CHOONI YENYE KITUNZIO CHAKE.**
- **SABUNI YA MAJI YA CHOONI LITA 4.**

3. **Sheria na kanuni muhimu za shule.**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

**3.1 Sheria na Kanuni za Shule**

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

**3.2 Makosa yatakayosababisha mwanafunzi kufukuzwa shule ni pamoja na:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule;
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xii. Kusababisha mimba;
xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

4. **Viambatanisho na fomu muhimu**

(a) Fomu ya uchunguzi wa Afya (Medical examination form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali. Fomu hii iambatanishwe na barua hii.

(b) Fomu ya maelezo binafsi ya kuhusu historia ya mwanafunzi au mkataba wa kutoshiriki katika mgomo, fujo na makossa ya jinai

(c) Fomu ya mzazi /mlezi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni, ulipaji wa michango na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.

(d) Picha (passport size) tano , 1 ya mwanafunzi ,zingine za wazazi au ndugu wa karibu wa mwanafunzi na namba zao za simu zinazo patikana.

(e) Nakala mbili ya cheti cha kuzaliwa (**2 copies of Birth certificates).**

(f) Nakala mbili za matokeo ya kitaifa ya kidato cha nne **( 2 copies of form IV National result slip**).

**NB:**

- **Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

  - **Mkuu wa shule**.............................................. **0629 155 082 / 0764 903 973**
  - **Makamu mkuu wa Shule....................... 0622 780 978 / 0767 184 204**
  - **Mwandamizi Taaluma ........................0623 785 672 / 0758 376 248**
  - **Mwalimu wa Nidhamu:**................................ **0626 144 239.**

## KARIBU SANA, SHULE YA SEKONDARI LUGUFU BOYS

MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI LUGUFU BOYS
S.L.P. 567
UVINZA - KIGOMA

**…………………………………**

**ISSA MOHAMED BYABUSHA**

**MKUU WA SHULE, SHULE YA SEKONDARI LUGUFU BOYS**

**OFISI YA WAZIRI MKUU– TAMISEMI**
**SHULE YA SEKONDARI LUGUFU BOYS**
**S.L.P 567 UVINZA KIGOMA**
**FOMU NAMBA 1**
**HISTORIA YA MWANAFUNZI**

1. Jina la Mwanafunzi ……………………………………………………………………………………………………..
2. Jina la Baba ……………………………………………………………………………………………………………
3. Jina la Mama …………………………………………………………………………………………………………..
4. Jina kamili la mlezi (kama hana mzazi)…………………………………………………………………………….
5. Anuani kamili ya Mzazi/Mlezi ……………………………………………………………………………………
6. Uhusiano wa Mlezi………………………………………………………(Mjomba/Shangazi/Kaka/Dada)
7. Kazi ya Baba/Mama/mlezi……………………………………… (Mkulima/Mfanyabiashara/Mfanyakazi)
8. Kama ni mfanyakazi ; kazi yake………………………………………………………………………………..
9. Kama ni mkulima ; zao muhimu analolitegemea ni ……………………………………………………………
10. Kama ni mfanya biashara; biashara yake ni ……………………………………………………………………
11. Afya yake (mwanafunzi) kama anayo matatizo ya kiafya na hivyo kustahili huduma maalumu. Tafadhali mzazi/mlezi eleza waziwazi …………………………………………………………………………….. ……………………………………………………………………………………………………………………
12. Dini na dhehebu la mwanafunzi……………………………………………………………………………
13. Majina ya wazazi/walezi na ndugu wengine wa karibu wa mwanafunzi na namba zao za simu;

| Jina kamili | Kazi yake | Namba ya Simu | Picha(passport size) |
|---|---|---|---|
| (1) ……………………………………… | ……………………….. | ……………………….. | |
| (2) ……………………………………… | ……………………….. | ……………………….. | |
| (3) ……………………………………… | ……………………….. | ……………………….. | |
| (4) ……………………………………… | ……………………….. | ……………………….. | |

**OFISI YA WAZIRI MKUU – TAMISEMI**

**SHULE YA SEKONDARI LUGUFU BOYS**

**S.L.P 567 UVINZA KIGOMA**

**FOMU NAMBA 2**

# FOMU YA KUKUBALI KUJIUNGA NA SHULE

## Sehemu (A)

(sehemu hii ijazwe na mwanafunzi mwenyewe)

Jina la mwanafunzi ………………………………………………………………………………………………………….

Jina la mzazi/mlezi……………………………………………………………………………………………………………

Anuani ya mzazi/mlezi………………………………………………………………………………………………………

Uhusiano………………………………………………………………(mjomba, shangazi, kaka, dada, bibi, babu)

Mimi ………………………………………………………………………………………… nikiwa nimechaguliwa kuwa mwanafunzi wa Tanzania naamini kuwa nimetunukiwa nafasi hiyo niliyopewa na umma wa Tanzania.

Hivyo ninaahidi kuwa nitajibidiisha kwa kadri ya uwezo wangu wote katika kazi zote nitakazopewa hapa shuleni nje na ndani ya darasa ili kuleta ufanisi. Endapo nitahusika katika uharibifu wowote wa mali za Shule nitawajibika kulipa mali hizo.

Ili kutimiza shabaha hiyo ninakubali na ninaahidi kwa hiari yangu mwenyewe kuwa nitafanya kazi kwa **Busara, Juhudi ya Hali ya Juu Kabisa na Kutii** kwa viongozi wote wa shule pamoja na sheria.

Nikiwa na maoni au malalamiko ninaahidi nitayafikisha panapohusika kwa njia na taratibu zinazokubalika.

Sahihi ya mwanafunzi …………………………………………………tarehe…………………………………………

## Sehemu (B)

(sehemu hii ijazwe na Mzazi/Mlezi)

Mimi ………………………………………………………………………………………. Mzazi/Mlezi wa mwanafunzi ……………………………………………………………………. Ninaahidi kuwa nitatimiza wajibu wangu kama mzazi/mlezi wa mtoto huyo kwa kushirikiana vema na uongozi wa shule.

Sahihi ya mzazi/mlezi …………………………………………………tarehe …………………………………………….

**OFISI YA WAZIRI MKUU – TAMISEMI**

**SHULE YA SEKONDARI LUGUFU BOYS**

**S.L.P 567 UVINZA – KIGOMA**

**FOMU NAMBA 3**

**MEDICAL EXAMINATION FORM**

To medical Officer I/C of ……………………………………………………………………………………………………

Designated Hospital, P.O. BOX …………………………………………………………………………………………

Please examine the above named in full as to his/per physical and mental fitness for being able to pursue two years of secondary school education. The examination should include categories (a) – (m).

In case of any acute or defect/ disability in each category or sub-category, may render the aspirant ineligible of admission or eligible of admission to schools of students with special needs.

(a) Pupil's name ……………………………………………………………………………………………………
(b) Age ……………………………………………………………………………………………………………..
(c) Stool test ……………………………………………………………………………………………………
(d) Blood group………………………………………………………………………………………………….
(e) Urine analysis……………………………………………………………………………………………….
(f) Syphilis test………………………………………………………………………………………………
(g) Chest test……………………………………………………………………………………………………
(h) Speech ………………………………………………………………………………………………………
(i) Eye test………………………………………………………………………………………………………..
(j) Abdomen …………………………………………………………………………………………………….
(k) Chest x-ray ………………………………………………………………………………………………
(l) Sickle cell test ……………………………………………………………………………………………..
(m) WCB total Differential ………………………………………………………………………………..

Additional information and physical defect or impairment to pursue further studies

……………………………………………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………………………………

Signed by ……………………………………………………………………………………………………………

Designation ………………………………………………………………………………………………………….

**……………………………………………………**

**Signature and Official stamp.**

# NB: VIPIMO VYOTE VIFANYIKE IPASAVYO NA FOMU HII IJAZWE KATIKA HOSIPITALI YA SERIKALI TU.

**FOMU NAMBA 4**

**OORODHA YA VITABU VYA MASOMO AMBAVYO MZAZI ANAWEZA MNUNULIA MWANAFUNZI KIMOJA WAPO AU ZAIDI KATIKA KILA SOMO.**

| VITABU | VITABU |
|---|---|
| **PHYSICS**<br>1. Nelkon and Parker, Advanced level Physics 7th edition.<br>2. S. Chand"s principles of physics class XI<br>3. S. Chand"s principles of physics ,class XII<br>4. Jim breithaupt, understanding physics 2nd / 4th edition<br>5. Roger Monastery, Advanced Level physics 4th edition<br>6. Tom Duncan, Advanced Level physics<br>7. Calculations , For Advanced level Physics<br>8. University Physics, New edition | **CHEMISTRY**<br>1. Physical chemistry, by Delungu (Mzumbe bookshop project 1998)<br>2. Advanced inorganic chemistry part I and II(Tanzania institute of education).<br>3. Organic Chemistry part 1, The fundamental principles I.L finar (longman LTD)<br>4. Conceptual Chemistry for class XI-Chand<br>5. Conceptual Chemistry for class XII-Chand |
| **GEOGRAPHY**<br>1. An integrated focal Regional study on Human and Economic Geography by.D.T.Msabila.<br>2. Physical Geography-D.T Msabila. | **BIOLOGY**<br>1. Biological science;Cambridge university press 1997 3rd edition<br>2. functional approach by Mbv Robert<br>3. New Understanding Biology By Suzan Toole<br>4. Advance biology Principles and application By C J Clegg and Mackean<br>5. Advanced Biology By Michael kent (2000).Oxford university press uk. |
| **ADVANCED AND BASIC APPLIED MATHEMATICS**<br>1. Basic applied Mathematics by Kiza and Septine I sillem<br>2. Advanced mathematics by shayo<br>3. Advanced Mathematics book 1 and 2 by Backhouse<br>4. Advanced Mathematics Chand's 1 and 2.<br>5. Advanced level pure Mathematics by C.J Tranter. | **HISTORY**<br>1. Essentials in advanced level History **by Saleh Yassin( 1&2)**<br>2. Advanced learners, History form V and six(history 1 and 2)( oxford 2011)<br>3. Advanced level History for Africa, From Neolithic Revolution to present(zist Kamili 2010)<br>4. Major events in the world History<br>5. Focus on Modern world history by Japhace, Ponsian, Chakupewa, Mpandije Yusuph P Maunda (2012 ) |
| **GENERAL STUDIES**<br>1. General studies for A- Level certificate form v<br>2. Contemporary approach for A level general studies notes for form v and six<br>3. General studies supplementary book for A level and colleges. | **ECONOMICS**<br>1. Economics for advanced level (1&2) by Ambilikile C.M<br>2. Essential of Economics 1&2 Ambros Odhiambo<br>3. Micro-economics by Dwiverd<br>4. Economics implified By N A Saleemi<br>5. Modern Economics By Robert Mudida. |
| **ENGLISH LANGUAGE.**<br>1. Introduction to Language-Nicholaus Ashery.<br>2. English for form V –Nyambari Nyangwine.<br>3. English Dictionary-Oxford. | **KISWAHILI**<br>1. Kamusi Ya Kiswahili Sanifu -TUKI<br>2. Nadharia Ya Fasihi Na Uhakiki -Masuko C Saluhaya<br>3. Nadharia ya Lugha Kidato Cha V & VI na elimu ya juu -Masuko C Saluhaya<br>4. Mising Ya Sarufi Ya Kiswahili- Karanja .P , J. Habwe na Na Masuko J.<br>Sarufi Fafanuzi Ya Kiswahili- Waihiga G |

**NB:**

1. Mwanafunzi wa somo la **Kiswahili lazima aje** na **Kamusi ya Kiswahili Sanifu-TUKI**.

2. Mwanafunzi wa somo la **Kingereza (English Language ) lazima aje** na **Kamusi ya Kingereza kwa kingereza ya Oxford.**